



MUHTASARI


- Hali ya ukavu inayotarajiwa inaweza kuathiri upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo.
- Mvua zinazotarajiwa kwa baadhi ya maeneo nchini hususan nyanda za juu kaskazini mashariki na pwani ya kaskazini zinaweza kufuatiwa na vipindi virefu vya ukavu na kuathiri uoteshaji na ukuaji wa mazao

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 11-20, 2021

Katika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) ilidhoofika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) haikuwa na mabadiliko makubwa. Hali hii iliendelea kusababisha upepo wenye nguvu ya wastani kuvuma kutoka kusini mashariki kuelekea maeneo ya pwani ya bahari ya Hindi. Hali ya Joto la bahari ya juu ya wastani mashariki na magharibi mwa bahari ya Hindi iliendelea kuleta mchango mdogo katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kuvuma kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani na hivyo kusababisha vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo hayo. Joto la bahari la juu ya wastani kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) lilipunguza kasi ya upepo uvumao kutoka misitu ya Kongo kuelekea magharibi mwa nchi.

MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 11-20, 2021

Katika dikadi hii vipindi vya mvua zaidi ya mm 26 vilirekodiwa katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi, pwani ya kaskazini, nyanda za juu kaskazini mashariki pamoja na nyanda za juu kusini magharibi kama inavyoonesha katika ramani.



Kielelezo 1: Kiasi cha mvua kwa kipindi cha Oktoba 11-20, 2021

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 11-20, 2021

Wakulima katika maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka waliendelea na shughuli za maandalizi ya mashamba kwa ajili ya msimu wa mvua za vuli isipokuwa katika mkoa ya Kagera na Mara ambako baadhi ya wakulima wameendelea kupanda mahindi, maharagwe na mhogo kwa kutumia mvua chache zilizonyesha katika maeneo hayo. Hata hivyo, baadhi ya mazao katika mkoa wa Kagera yameripotiwa kuathirika kutokana na vipindi virefu vya ukavu.

Kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka baadhi ya wakulima waliendelea na uandaaji wa mashamba kwa ajili ya mvua za msimu.

HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 11-20, 2021

Katika dikadi hii, kina cha maji katika mabwawa, mabonde na mtiririko wa maji kwenye mito viliendelea kupungua hususan maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kutokana na hali ya ukavu iliyoendelea.

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 21-31, 2021

Katika dikadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) ilipungua nguvu wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilionesha mabadiliko kidogo. Hali hii iliendelea kusababisha upepo wenye nguvu ya wastani kuvuma kutoka kusini mashariki kuelekea maeneo ya pwani ya Bahari ya Hindi. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani lilionekana mashariki mwa bahari ya Hindi wakati magharibi mwa bahari ya Hindi joto la bahari lilikuwa la wastani. Hali hii iliendelea kuleta mchango mdogo katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kuvuma kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani na hivyo kusababisha vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo hayo. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani lilionekana upande wa kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) na hivyo kupunguza kasi ya upepo uvumao kutoka misitu ya Congo kuelekea magharibi mwa nchi.

HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 21-31, 2021

Kanda ya Ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) na pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) yanatarajiwa kupata vipindi vichache vya mvua nyepesi.

Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) na kanda ya kusini (mikoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KIPINDI CHA OKTOBA 21-31, 2021

Mvua zinazotarajiwa kwa maeneo ya ukanda wa pwani pamoja na nyanda za juu kaskazini mashariki zinaweza kufuatana na vipindi virefu vya ukavu na kuathiri uoteshaji wa mazao katika maeneo hayo.

Pia, hali ya ukavu inayotarajiwa inaweza kuathiri upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo.

Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa wataalamu wa sekta husika. Pia, inashauriwa kuendelea kufuatilia utabiri wa hali ya hewa wa kila siku, siku tano na tahadhari kadri zinavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania nchini (TMA).

HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 21-31, 2021

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kupungua hasa katika maeneo yanaopata mvua mara moja kwa mwaka kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa. Hivyo, wananchi na mamlaka husika wanashauriwa kutumia rasilimali maji kwa uangalifu.